Taarifa kwa vyombo vya habari
Imezuiwa hadi 19 Decemba2012 saa 5 asubuhi

Wakazi wa Dar es Salaam hawaridhishwi na hali ya utoaji wa huduma, hawana imani na taasisi za umma na hawazielewi vizuri sera

Wapo walioripoti kuchukua hatua ili kubadili hali zao

19 Decemba 2012, Dar es Salaam: Wakazi wa Dar es Salaam hawaridhishwi na viwango vya utoaji huduma za jamii, waelezea jinsi rushwa inavyozidi kukithiri na hawana imani thabiti kwa taasisi za umma na viongozi wanaopaswa kuwawakilisha na kuwatumikia. Viwango vya kutoridhishwa na jinsi utoaji huduma za jamii unavyosimamiwa ni vya juu sana. Kati ya asilimia 60 na 80 ya wakazi hawafurahii jinsi huduma za afya; maji; miundombinu ya maji taka zinavyoshughulikiwa. Utoaji wa huduma ya umeme wa uhakika ulipewa nafasi ya juu zaidi kulinganisha na huduma hizo nyingine nne, kukiwa na zaidi ya asilimia 50 ya wakazi wa Dar es Salaam waliosema kuwa huduma hiyo inashughulikiwa vema.

Matokeo haya yametolewa kupitia muhtasari wa uchambuzi wa sera uliofanywa na Uwazi—Twaweza uliopewa jina la *Dar es Salaam wanachukuliaje utawala? Maoni ya watu kuhusu huduma, sera na viongozi.* Muhtasari huo wa sera umetokana na taftishi iliyoendeshwa katika kaya 550 mwezi Agosti hadi Septemba, 2010. Taftishi hiyo iliendeshwa katika wilaya za Ilala, Kinondoni na Temeke. Wahojiwa waliulizwa maoni yao kuhusu hali ya utoaji wa huduma na jinsi walivyojishughulisha kutatua masuala yaliyowagusa.

Walipoulizwa kuhusu viwango vya imani yao kwa utayari wa taasisi za umma kushughulikia mambo yanayougusa umma, washiriki walionyesha kuwa na imani zaidi na mahakama na polisi kuliko Kampuni ya Dar es Salaam ya Maji na Maji Taka (DAWASCO) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Ni asilimia 29 tu ya wakazi wa Dar es Salaam ndiyo kwa kiasi fulani wana imani na DAWASCO kuweza kutenda mambo kwa kuzingatia mahitaji ya umma, wakati ambapo asilimia 65 ya watu hao wana imani na mahakama na asilimia 62 wanaamini polisi wanaweza kutimiza wajibu wao kwa umma. Kwa ujumla, imani kwa viongozi mmojammoja iko juu zaidi kuliko imani kwa taasisi. Kwa mfano, asilimia 91 ya wahojiwa walieleza kuwa na imani na viongozi wa dini na asilimia 84 walisema wana imani na Rais. Viongozi waliopata asilimia za chini zaidi katika kuaminiwa, hata hivyo, ni Wabunge, ambapo ni asilimia 44 tu ndiyo walisema wanaamini kwamba wawakilishi wao hao wanashughulika kwa maslahi ya umma mzima.

Wakati huo huo, karibu asilimia 60 ya wahojiwa wanafikiri kwamba rushwa umekithiri zaidi kulinganisha na miaka mitano iliyopita. Karibu watu watatu kati ya kumi walisema walilazimika kutoa rushwa ili kupata huduma iliyopaswa kutolewa bila malipo katika vituo vya afya katika kipindi cha miezi 12 kabla ya

taftishi kufanyika, wakati ambapo mmoja kati ya kumi alisema alitoa rushwa kwa polisi katika kipindi hicho hicho.

Taftishi pia ilionyesha kwamba kulikuwa na uelewa mdogo kuhusu sera na vipaumbele vywa taifa, na kuhusu wawakilishi wa wananchi katika masuala ya kisiasa. Zaidi ya asilimia 70 ya wahojiwa hawakuwahi kusikia kuhusu au walishindwa kuelezea MKUKUTA, Kilimo Kwanza na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vilevile, karibu nusu ya wakazi wa Dar es Salaam waliohojiwa walikuwa hawajui majina ya Wabunge wao.

Licha ya viwango vya juu vya kutoridhishwa hali ya utoaji wa huduma za jammi na kutokuwa na imani, wakazi wa Dar es Salaam hawakuonyesha, katika taarifa walizotoa, kuwa na ari kubwa ya kuchukua jukumu la kuleta mabadiliko katika matokeo ya utoaji wa huduma. Hofu ya kuadhibiwa huenda ni moja ya sababu. Karibu asilimia 40 ya washiriki wa taftishi walisema wanafikiri kulikuwa na uwezekano wa kuadhibiwa kwa kukemea utoaji wa huduma mbovu. Kwa ujumla, wahojiwa wa taftishi waliripoti kuchukua hatua katika vikundi zaidi kuliko kama mtu mmojammoja. Njia zilizotumika sana katika hili ni kushiriki kwenye mijadala ya mitaani (48%); kushiriki mikutano ya jamii (59%) na mikutano ya kamati za shule (40%). Kwa upande mwingine, ni asilimia 8 tu ya wahojiwa ndiyo waliozungumzia masuala ya jamii kupitia njia za kawaida za mawasiliano na asilimia 10 walipiga simu kwenye vipindi vya redio. Sababu nyingine ya ari ndogo ya kuchukua hatua kushughulikia masuala yasiyoridhisha inaweza kuhusishwa na hali ya wananchi kutojua njia/fursa na nyenzo zilizopo na zilizo wazi kwao, au ile imani ya kwamba huenda ushiriki wao unaweza usibadilishe chochote.

Mushi Elvis wa Twaweza anaeleza kwamba *'Utoaji wa huduma ulio duni ni suala ambalo serikali haina budi kulishughulikia kama jambo la kupewa kipaumbele. Hata hivyo, kama raia, tuna haki na wajibu wa kuhakikisha kwamba tunafanya sehemu yetu, kwa kuzisoma na kuzifahamu sera na vipaumbele vya kitaifa, kuweka wazi masuala tunayokabiliana nayo, na kuwasiliana na viongozi na taasisi zinazotuwakilisha ili watambue maoni/mitazamo yetu.'*

Viwango vya juu vya imani walivyo navyo wananchi kwa Rais na viongozi wa dini, vinatoa fursa muhimu ya kushughulikia baadhi ya changamoto zilizopo katika utoaji wa huduma. Lakini kuhamasisha njia mbalimbali za ushiriki wa wanachi ndiyo ufunguo muhimu. Kila sehemu ya jamii, kuanzia serikali hadi viongozi wa dini, wana wajibu wa kutimiza katika kuhakikisha ufanisi na kutolewa kwa huduma bora nchini Tanzania. Bila shaka kunaweza kuwepo mabadiliko pale wenye mamlaka wanapoelewa kwamba watawajibishwa kwa kushindwa kwao kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

---- Ends ----

Kwa taarifa zaidi:
Risha Chande
Afisa Mawasiliano na Utetezi, Twaweza
Barua pepe: rchande@twaweza.org | **simu:** (+255) (0) 656 665 7559

Matini kwa Wahariri

- Data kamili kutoka Taftishi ya Uwazi kuhusu Utoaji wa Huduma inaweza kupatikana katika www.listeningtodar.org.

- Twaweza ni mpango wa miaka kumi unaolenga kuleta mabadiliko makubwa katika Afrika Mashariki. Twaweza ina-amini kwamba mabadiliko ya kudumu yanahitaji kutoka kwa wananchi wenyewe “bottom-up”, na inajishughulisha kuendeleza hali na kupanua fursa ambazo kwa kupitia hizo mamilioni ya watu wanaweza kupata habari na kuleta mabadiliko katika jamii zao moja kwa moja na kwa kuiwajibisha serikali.
- Uwazi iliyoko Twaweza inatoa na kusambaza takwimu na taarifa muhimu ili kufahamisha mijadala ya umma. Dhamira ya Uwazi ni kuwawezesha walengwa wakuu kupata taarifa za kuaminika, kwa wakati, na chambuzi zinazoeleweka kwa urahisi ili kuboresha mijadala ya umma na kuchangia katika kuinua uwajibikaji na ushiriki wa wananchi.
- Unaweza kufuatilia kazi ya Twaweza kwenye
  Tovuti: www.twaweza.org **Ukurasa wa Facebook:** Twaweza Tanzania **Anwani ya Twitter:** @Twaweza_NiSisi